MWITO PROG 1091 KISWAHILI SCRIPT

SCRIPTURE:ROMANS 5:17

TRANSWORLD RADIO

INTRO:

Nakukaribisha tena msikilizaji wangu kwa kipindi cha MWITO nambari 1091 kutoka studio zetu za Nairobi.Sina shaka kwamba Mungu amekulinda na hata kukufikisha siku ya leo ambapo tunakutana tena.Nakukumbusha kuwa kipindi hiki kinakujia kwa hisani na udhamini mkubwa wa huduma ya kimataifa ya Macedonian Call yake Harod Williams.

Tunaendelea na mfululizo wa somo letu kutoka kitabu cha Warumi sura ya 5.Na jinsi nilivyotangulia kusema madhumuni ya kipindi hiki ni kukuhamasisha uwe miongoni mwa wale watakaoshuhudia na hata kueneza injili ya wokovu ya Yesu Kristo.Kabla ya kuendelea hebu nikukumbushe kuwa kwenye kipindi kilichopita tulisoma aya ya 15 kama msingi wa somo letu.Hebu tusome aya ya 14 kisha ile ya 15 kama msingi wa somo letu…..….. ***walakini mauti ilitawala tangu Adamu mpaka Musa nayo ilitawala hata wao wasiofanya dhambi ifanayayo na kosa la adamu aliye*** mfano ***wake yeye atakayekuja.Lakini karama ile haikuwa kama lile kosa;kwa maana ikiwa kwa kukosa kwake yule mmoja wengi walikufa zaidi sana neema ya Mungu na kipawa kilico katika neema*** yake ***mwanadamu mmoja Yesu Kristo kimezidi kwa ajili ya wale wengi.***

Mpendwa msikilizaji ni wakai mwingine tena ambapo nakuletea somo la leo kutoka kitabu cha Warumi.Naamini una kalamu na karatsi ili kuandika yale ya muhimu kutokana na somo la leo.Kwenye kipindi kilichopita tuliachia mahala muhimu sana.Swala la wokovu kwa binadamu wote.Kuna wengi wanodai kuwa kwa sababu

Adamu alitenda dhambi na sote tukakawa watenda dhambi kw urithi,basi ikiwa Yesu alitufia sote basi tumeokoka sote pia.Lakini ni waummishi wachache waliofuniliwa ukweli ambao watangámjua kuwa ndiyo Yesu alifia wote ,lakini wokovu ni kwa wale watakaomkiri kwa kutubu dhambi zao na kuokolewa kwa damu ya Yesu Kristo,ambao kwa hakika wataepuka mauti kutokana na dhsambi ya urithi ya adamu.Wale wanaomwamini kuwa Yesu ni mwana wa Mungu na alilipa deni la dhambi za binadamu msalabani pale golikotha.Hata hivyo hakuna kitu kama wokovu kwa binadamu wote ,jinsi wengine wangependa kujiaminish.Ukweli ni kwamba wae ambao majina yao hsyatskuwa kwenye kitabu cha uzima watatupwa kwenye ziwa la moto wa kiberiti.Isitodhe kunao wasomi wa thilojia ambao wamedanganya wengi kwamba sote tumeokokolewa kutokana na tendo la Yesu kufa msalabani,wala hapa jingne tunalohitajika kufanya.Kwamb Mungu mwenye upendo hawezi kuwaadhibu wanawe.wengi hawafurahii ukweli kwamba Mungu mwenhe upando anaweza kuruhusu vuymbe wake wateketee kwenye moto wa kuzimu.Ndiposa kutokana na injili potofu wengi wa manabii na walimu hao wa uwongo wameficha vichwa vyao mavumbini jinsi afnyavyo mbuni na kujisahaulisha kuwa kuna ziwa la moto kwa watenda dhambi.Lakini ukweli ni kwamba kujidanganya kuwa hali fulani haipo ,hakusaidi lolote ,kwa kuwa hali halisi ipo na itasalia kuwepo.

Mpendwa hebu nikwambia kuwa ikiwa hujaokoka na ungali unaishi maisha ya dhambi,hakika hukumu ya kifo yakungoja.Utatengwa daima na muumba wako na kutupwa jehenamu.Jehenamu kumetengewa wenye dhambi ambao wamefanya shingo ngumu na hawajaokoka licha ya mahubiri mengi ambayo wamesikia.Hiyo ndiyo gharama ambayo watalipa kwa kutomkubali Kristo ambaye tayari amelipia kikamilifu deni la dhambi.Baada ya hakikisho la kulipia deni la dhambi Kristo alifufuka katika wafu na sasa yuko kono wa kuume waMungu akituombea.Ansema

njjooni kwangu enyi mliolemewa na mizigo name nitawapumzisha.Anasema nira yake ni nyepesi.Maandiko yansema kuwa binadamu ametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.Mchakato mzima unahusu mateso, kifo cha Yesu na uhesabiwaji haki.Ambapo tunahesabiwa kuwa wana wa Mungu.Huo ni upendo mkubwa kwa hakika.Rafiki yanu baada ya ufafanuzi huo huna kisababu cha kutompokea kristo kuwa mwokozi wako.Na ikiwa utaendelekea kufukia kichwa chako mchangani afanyavyo mbuni,basi utajilaumu mwenyewe.Naam nitairejelea tena ya ya 17 ya Warumi sura ya tano… ***kwa maana ikiwa kwa kukosa mtu mmoja mauti yalitawala kwa sabbu ya yule mmoja,zaidi sana wao waokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki watatawala katika uzima kwa yule mmoja,Yesu kristo.Hebu tuendelee na aya ya 18……Basi tena kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu,kadhalika kwa tendo moja la haki,watu wote walihesabiwa haki yenye uzima.Kwasababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi,kadhalika kwa kutii kwake mmoja,wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki.*** Naam maandko yanasema kutokana na msamaha wa mmoja wengi watasamehewa.Wale waliompokea Yesu kristo,kwa imani kuwa mwokozi wao wamehesabiwa haki .Kumbuka kuwa baba wa imani Ibrahimu alihesabiwa haki kwa kumwamini Mungu.Naomba nikamilishe somo hli kwa leo kwa kukuuliza swali rahisi sna.Umeshmpokea Krio kuwa mwokozi wakozi wako? Una uhakika ni wapi utaishi maisha yako ya umilele.Itakuwa kwenye mateso kule jehenamu au na Kristo huko Paradiso.?

Una hakika utamwona Kristo atakapordi kuwachukua walio wake? Wale ambao wameokoka na wanafanya kazi yake? Fursa ni hii ikiwa hujamjua Kristo kuwa mwokozi wako.Tubu dhambi zako sasa n umwendee ndugu u dada aliyeokoka na ushiriki naye kuhusu uamuzi uliofanya.Aidha mwendee mchungaji wa kanisa

linalohubiri wokovu wa Yesu Kristo.Atakushauri na kukuelekeza jinsi ya kukuza imani yako. ? nambari ifwatayo-: 0721 970 520. Au 020 2679842.Ikiwa unaishi Nairobi Utamfungulia mlango wa moyo wako ili apate kuingia?Ikiwa jibu lako ni ndio ningependa utubu dhambi zako leo na kumpokea rohoni mwako ili akue dira mpya maishani mwako.Usije ukatahayari siku ya mwisho,wakati wateule wake watakapopanga foleni kuingia Jerusalemu mpya.Mbinguni ambako tumeandaliwa makao.Chukua hatua hiyo sasa hivi.Ninasubiri uchukue hatua hiyo ,kisha uniandikie au unitumie ujumbe mfupi.Nitafurahi sana kuwasiliana nawe na ahata kukupatia vijitabu nan akala ya agano jipya la Bibilia kukusaidia kuweka msingi imara wa ukristo wako. Zaidi ya hayo.Nitafurahi sana nitakapopokea maoni yako kukihusu kipindi hiki na hasa jinsi ya kukifanya kiwe cha manufaa zaidi kwako.Hiki kimekuwa kipindi cha Mwito nambari 1091 Naomba uwasiliane nami kupitia njia ya arafa ukitumia tunakukaribisha ututembelee kwenye studio zetu za TWR Kamburu Drive,off Ngong Road, baada ya jumba la TOP PLAZA.Anwani yangu ikiwa utaniandikia barua ni-:Kwa mtayarishi,Mwito,S.L.P.21514-00505 Nairobi.Waweza pia kuwasiliana nami kwa njia ya barua pepe ifwatavyo-barua@twr.co.ke.Na basi kufikia hapo sina budi kulikunja jamvi langu kwa leo ninapokutakia baraka sufufu kutoka kwake Mungu wetu mtukuka.Juma lijalo tutaingia aya ya 19 ya sura ya pili ya kitabu cha Warumi.Ni mwaandazi wa kipindi hiki ndugu Charles Otunga ninayekuaga nikikutakia mbawazi zake Mungu wetu mtukuka.Kwaheri.

xxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxx